JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3
Fax Na: 2152820
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Kamishna wa Mamlaka )*

08 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 80327,
**DAR ES SALAAM.**

## TAARIFA KWA UMMA

KAMPUNI YA TECHNO NET SCIENTIFIC YAKIRI KOSA LA KUFANYA BIASHARA YA KEMIKALI BILA KIBALI

Dar es Salaam, 24 Desemba, 2019:

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaamuru wakurugenzi na wafanyakazi wa kampuni ya **TECHNO NET SCIENTIFIC** kulipa faini ya shilingi laki tano kila mmoja, na fidia ya shilingi milioni mia moja (100) kwa kosa la kujihusisha na biashara ya kemikali bila kuwa na usajili. Wafanyakazi waliofikishwa mahakamani na kusomewa adhabu hiyo ni Benedict Gabriel Assey, Wenceslaus Aloyyce Assey, Winfrida Mbelesero Assey, Salvatory Benedict Assey, Emmanuel Benedict Assey, Samwel Mlekwa Mahalila na Matilda Peter Temba.

Vilevile mahakama imetoa amri ya kutaifisha kemikali zote zilizokamatwa kuhusiana na shauri hilo na kuelekeza ziwe chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Amri hizi zimetolewa kufuatia makubaliano ya kukiri kosa yaliyofanywa baina ya washtakiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Ikumbukwe kuwa hivi karibuni Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini ilikamata kemikali bashirifu zenye ujazo wa lita 6,494 zilizokuwa zikimilikiwa na kampuni ya **TECHNNO NET SCIENTIFIC** isivyo halali. Sheria zilizokiukwa ni Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, sura ya 95 na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya mwaka 2003.

Kemikali bashirifu zinaweza kutumika kihalali viwandani na hospitalini, lakini watu wenye nia ovu wanaweza kuzitumia kutengeneza dawa za kulevya. Vilevile kemikali hizi zinaweza kuzalisha taka zenye sumu ambazo zinaweza kuhatarisha afya za watu na kuchafua mazingira. Hivyo, utaratibu wa udhibiti umewekwa kuanzia hatua ya ununuzi, usafirishaji, uhifadhi na utumiaji.

Washtakiwa wote saba wameshalipa faini pamoja na fidia, shauri limepangwa kwa kutajwa tarehe 16/01/2020 dhidi ya mshtakiwa wa nane (8) ambaye alikana mashtaka.

Imetolewa na,

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**